JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAASISI YA UONGOZI

UONGOZI Institute

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## KONGAMANO LA WANAWAKE KATIKA UONGOZI KUFANYIKA KWA MARA YA TANO

**6 Oktoba 2025:** Kongamano la Wanawake katika Uongozi la Taasisi UONGOZI litafanyika leo kwa mara ya tano Jijini Dar es Salaam, chini ya dhima ya "*Mchango wa wanawake katika uongozi barani Afrika*".

Mgeni Rasmi wa Tukio hili atakuwa Dkt. John Jingu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Tanzania). Wasilisho kuu litatolewa na Dkt. Linda Ncube-Nkomo, Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Watoto ya Nelson Mandela (Afrika Kusini).

Tukio hili linafanyika kama sehemu ya Programu ya Uongozi kwa Wanawake (*Women's Leadership Programme*) ya Taasisi ya UONGOZI, yenye lengo la kukuza nafasi za uongozi kwa wanawake. Programu hii ya miezi sita inajumuisha kongamano, mafunzo ya mfululizo ya siku sita, pamoja na ushauri mahususi wa kukuza sifa za uongozi. Utekelezaji wa programu hii unawezeshwa kwa kiasi kikubwa na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Finland, pamoja na Umoja wa Ulaya.

Wageni watakaohudhuria ni pamoja na viongozi waandamizi kutoka nchi mbalimbali duniani na sekta zote ikiwemo sekta ya umma, sekta binafsi, sekta ya elimu ya juu, na sekta ya asasi za kiraia; pamoja na wanawake 100 waliochaguliwa kujiunga na Programu ya Uongozi kwa Wanawake.

Ushiriki katika tukio hili ni kwa mwaliko pekee.

Imetolewa na,

Suzana Aroko

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma**

UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
Kura Yako Haki Yako Jitokeze
Kupiga Kura